**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

1993

# Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof.Kighoma A.Malima, Mbunge, wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka, 1993-1994

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/794

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

DEVPLAN LIBRARY
P. O. Box 9242
DAR ES SALAAM
Tanzania.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Kighoma A. Malima, Mbunge, wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 1993/94

1993
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM—TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA PROF. KIGHOMA A. MALIMA MBUNGE WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 1993/94

Mheshimiwa Spika,

Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kujadili makusudio na shabaha za makadirio ya matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 1993/94.

## Utangulizi

2. Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Juni Mwaka huu niliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Bajeti ya Serikali kwa jumla kwa mwaka 1993/94. Bajeti hiyo ndiyo imekuwa msingi wa Bunge hili kuchambua, kujadili, na hatimaye kuidhinisha bajeti ya kila Wizara. Leo nina heshima kuwasilisha makisio na shabaha zilizomo katika makadirio ya matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 1993/94 ili yapate idhini ya Bunge lako tukufu.

## Majukumu Ya Wizara Ya Fedha

3. Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, majukumu ya Wizara ya Fedha ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kukusanya na kudhibiti mapato ya Serikali yanayoidhinishwa na Bunge kwenye sheria mbalimbali.

(ii) Kudhibiti matumizi ya Serikali kwa kuhakikisha kuwa sheria na kanuni zilizowekwa zinazingatiwa na wote wanaohusika.

(iii) Kuratibu na kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za kigeni zitokanazo na mauzo yetu nje pamoja na misaada na mikopo kutoka nje.

(iv) Kudhibiti Mitaji ya Serikali katika Mashirika ya Umma kwa lengo la kuleta ufanisi na faida.

(v) Kudhibiti na kuratibu taasisi za fedha nchini.

(vi) kusimamia sera za uhasibu na ukaguzi nchini.

(vii) Kusimamia deni la taifa katika ujumla wake.

(viii) Kubuni na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa watumishi wake katika fani za fedha, ukaguzi wa hesabu, uhakikimali, kampyuta na kodi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wataalam na kuongeza ufanisi katika sekta hii.

4. Mheshimiwa Spika, napenda tangu awali nitamke kuwa Wizara yangu hutekeleza majukumu niliyayataja kwa ushirikiana wa karibu na Wizara zote, na taasisi nyingine za Serikali.

Pia hushirikiana na kupata mchango mkubwa wa Bunge lako tukufu kupitia Kamati ya Bunge ya Mahesabu (PAC), Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POC) na Kamati ya Fedha na Uchumi. Kamati hizi sasa zinaongazwa na Waheshimiwa Yusufu Mahmoud, Mbunge wa Kwamtipura, Nasoro Malocho Mbunge wa Newala, na Mathias Kihaule Mbunge wa Ludewa. Hivyo ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizo kwa kazi nzuri wanayofanya katika kufichua kasoro za utendaji na kushauri juu ya hatua za kuboresha shughuli za kifedha na uchumi wetu kwa ujumla. Kwa hakika wanastahili pongezi zetu wote.

5. Mheshimiwa Spika, ni azma ya Wizara ya Fedha kuendelea kushirikiana na Bunge hili pamoja na Kamati zake zote katika mwako 1993/94 katika kudhibiti fedha na mali ya Serikali ili zitumike kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Baada ya kueleza hayo na kwa kuzingatia kuwa masuala mengi yalijadiliwa wakati nikiwasilisha mapendekezo ya Bejeti ya Serikali mwanzoni mwa kikao hiki, ni nia yangu kueleza kwa muhtasari tu mapitio ya utekelezaji wa malengo na shabaha kwa Mwaka 1992/93 na malengo na shabaha kwa Mwaka 1993/94.

## Fedha za Kigeni.

6. Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1992/93 Wizara yangu imeendelea na juhudi zake za kutafuta na kudhibiti misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wa nje na vyombo vya fedha vya Kimataifa. Kwa upande wa misaada na mikopo kutoka nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo, matarajio kwa mwaka 1993/94 ni dola za Kimarekani 261.3 milioni ukilinganisha na mapato ya dola za Kimarekani 129.3 milioni mnamo 1992/93. Aidha, misaada na mikopo toka nje kwa ajili ya kusaidia uagizaji wa bidhaa (CIS & OGL) inatarajiwa kuwa dola za Kimarekani 271.8 milioni ukilinganisha na dola za

Kimarekani 347.8 milioni mnamo 1992/93 na dala za Kimarekani 295.3 milioni mwaka 1991/92. Ni matumani yetu kuwa wahisani watachangia kama walivyoahidi na kwa wakati uliopangwa ili kutoathiri shughuli zilizokusudiwa.

7. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1992/93 shughuli za kudhibiti na kuratibu Madeni na Mikopa ziliendelea kutekelezwa. Wizara pia iliendelea kuwafuatilia wote wanaodaiwa chini ya utaratibu wa" Cammadity Import Suppart". Katika kulishughulikia suala hili, Wizara yangu iliunda Kamati Maalum ya Wataalam iliyashirikisha idara zinazohusika pamoja na Mabenki ili kuchunguza na kuhakiki madeni yanayadaiwa Wizara, Mashirika ya Umma, Vyama vya Ushirika, na Watu Binafsi. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati hiyo tayari imetoa taarifa yake ambaya Wizara inaifanyia kazi. Kulingana na taarifa hiyo baadhi ya Madeni, ambaya hayajathibitishwa na wadaiwa, kwa kipindi cha 1987/88 hadi 1992/93 ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara na idara za Serikali 15 zinadaiwa Sh. 8,189,274,622/=

(ii) Mashirika na Vyama 92 yanadaiwa Sh. 70,850,855,387/=

(iii) Makampuni Binafsi 179 yanadaiwa Sh. 31,546,420,628/=

Wadaiwa wote hawa wanaendelea kushughulikiwa na Kamishna wa Kodi ya Mapato chini ya Sheria Na. 15 ya 1992 kwa madhumuni ya kukusanya madeni haya.

**Madeni na Uratibu wa Misaada**

8. Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kushughulikia Deni la Taifa, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kuweka mikakati ya kupunguza deni letu la nje ambalo hadi kufikia mwishoni mwa Juni 1992 lilifikia dola za Kimarekani 6,400 milioni.

Kwa sababu ya ukubwa wa deni hili Wizara inachukua hatua mbalimbali za kuimarisha uratibu na udhibiti wake kwa lengo la kuwa na taarifa sahihi na pia kupunguza kasi ya ukuaji wake. Kutokana na juhudi hizo, kuanzia mwaka 1986 hadi sasa nchi kadhaa zinazotudai zimeweza kufuta madeni yao kwetu yenye thamani ya dola za Kimarekani 453.08 milioni. Madeni mengine yenye thamani ya dola za Kimarekani 29.69 milioni yalifutwa chini ya mpango wa "Paris Club". Pia tumeendelea kupata unafuu mwingine wa kuahirishiwa ulipaji wa madeni yaliyopevuka mwaka 1986 dola 713.0 milioni, mwaka 1988 dola 377.0 milioni, mwaka 1990 dola 200 milioni, na mwaka 1992 - 1994 dola 698 milioni.

9. Mheshimiwa Spika, utaratibu mwingine ambao ulisaidia kupunguza madeni yetu ni ule wa uwekezaji wa mitaji ya madeni nchini (Debt conversion for Investment Programme). Chini ya mpango huu, mdai anaweza kuliuza deni hilo kwa bei nafuu. Mpango wa kuuza madeni kwa wawekezaji vitega uchumi una malengo yafuatayo:-

(i) kukuza uwekezaji rasilimali katika sekta muhimu kama vile Kilimo, Utalii, Viwanda na Madini

(ii) kupunguza limbikizo la madeni.

Madeni yaliyouzwa chini ya mpango huu ni pamoja na;-

(a) Malimbikizo ya malipo yanayotokana na mikopo ya mabenki, biashara binafsi na "suppliers credits"

(b) malimbikizo ya malipo yatokanayo na uhamishaji wa fedha za mashirika ya ndege, malipo ya wataalam wa kigeni, n.k.,

(c) Malimbikizo ya madeni ya Serikali. Katika kipindi cha 1992/93 miradi yenye thamani ya

dola za Kimarekani 72.84 milioni iliidhinishwo na madeni yenye thamani ya dola za Kimarekani 29.41 miliani yalikuwa yamenunuliwa na kubadilishwa.

10. Mheshimiwa Spika, kutakana na utekelezaji wa mpango wa kurekebisha uchumi (ESAF II) ambao Serikali inautekeleza kwa kushirikiana na Benki ya Dunia unofuu wa madeni unaotokana na uwekezaji mitaji nchini (Debt Canversian) utaachwa na badala yake utaratibu wa "Debt BuyBack" utatumika kuanzia mwaka 1993/94. Chini ya mpango huu Benki ya Dunia pamaja na wahisani kadhaa watachangia fedha kwenye mfuko maalum ambao utaiwezesha Tanzania kununua madeni yake ya kibiashara yanayokadiriwa kufikia dala za Marekani zipatazo milioni 200. Inategemewa utekelezaji wa mpanga huu utaleta faida zifuatazo:-

(i) Kupunguza mzigo wa madeni sugu ya nchi yetu kwa wafanyabiashara wa kigeni,

(ii) kurejesha hadhi ya nchi kibiashara kwenye masoko ya kimataifa (credit worthiness) ili kuweza kufufua biashara kwa mikopo ya muda mfupi na masharti nafuu. Hali hiyo itatuwezesha kujipenyeza kwa urahisi zaidi katika masoko ya fedha ya kimataifa (capital markets) kwa ajili ya kuongeza uwekezaji rasilimali nchini,

(iii) kupunguza madeni ya nchi bila kuleta madhara ya mfumuko wa bei,

(iv) kuwa kichocheo kwa wawekezaji rasilimali toka nje,

(v) kurahisisha usimamizi wa madeni kwa ujumla.

11. Mheshimiwa Spika, ili kupata taarifa zilizo sahihi za misaada itolewayo no wahisani, wizara yangu imeandaa mradi utakaohisaniwa na UNDP wa kuratibu takwimu za misaada kwenye sekta zetu zote. Mradi huu unaaitwa "Aid Managemenent, Administration and Coordination Systems" (AMACS) utatupatia mwelekea wa kutumia misaada tunayoipata na kuondokana na "duplication" ya misaada hiyo kwenye miradi yetu ya maendeleo. Mradi huu utatekelezwa mwaka huu wa fedha (1993/94).

Mapato ya Serikali.

12. Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali hutokana na Idara za kodi zilizo chini ya Hazina, Wizara na Mikoa. Sehemu kubwa ya mapato hayo huingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Exchequer) na mengine kama vile mapato au "Appropriation-In-Aid" hukusanywa na kutumiwa moja kwa moja na taasisi zinazohusika.

Katika mwaka 1992/93, Serikali ilikadiria kukusanyo jumla ya Sh. 215,607 milioni. Kati ya kiasi hicho, Sh.196,583 milioni zilitegemewa kutokana na kodi mbalimbali zinazokusanywa na Idara za Kodi na Sh.19,024 milioni kutoka vianzio vingine.

13. Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka huu Serikali imefanya marekebisho katika muundo wa Idara zake za Kodi. Katika marekebisho haya Idara ya Forodha na Kodi ya Mauzo imegawanywa na kuwa Idara za Forodha, Idara ya Kodi ya Mauzo na Idara ya Upelelezi. Lengo la mabadiliko hayo ni kuimarisha na kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kabla ya kuvunjwa kwa Idara ya Forodha na Kodi ya Mauzo, Idara hiyo katika mwaka 1992/93 ilikuwa imepangiwa kukusanya mapato ya Serikali ya kiasi cha Sh.159,215 milioni, kutokana na vianzio mbalimbali. Taarifa za awali zinaonyesha kuwa hadi kufikia Machi, 1993 makusanyo yalifikia Sh.71,543 milioni au asilimia 45 ya kiasi kilichopangwa kukusanywa.

Kutokana na mwenendo huu wa makusanyo, Idara ilitegemea kukusanya Jumla ya Sh.107,869 milioni hadi mwishoni mwa Juni, 1993, hivyo kuwa nyuma ya lengo kwa Sh.51,346 milioni au asilimia 32. Hali ya makusanyo katika mwaka wa fedha 1992/93 haikuridhisha pomoja na Jitihada kubwa za Idara za kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika maeneo yote kwa "Tax Campaign" na utaratibu wa kuweko maofisa wakazi kwenye viwanda vikubwa nchini hosa vyenye mapato makubwa na udhibiti wa bidhaa zote zinazouzwa nje ya nchi na zile zinazoagizwa.

## <u>Idara ya Forodha</u>

14. Mheshimiwa Spika, Idara mpya ya Forodha itakuwa na majukumu yo kukusonya mapato ya Serikoli kutoko kotika vionzio mbalimbali koma Ushuru wa Forodha kwa bidhaa zinozoagizwa kutoka nje, pamoja na kodi nyingine. Aidha, Idara itahusika no udhibiti wa biashora ya nje (import & Exports) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali.

15. Mheshimiwo Spika, kotiko mwaka 1993/94 Idoro yo Forodho imepongiwa kukusanyo Sh.38,900 milioni omboyo ni Sh.3,601 milioni, ou asilimio 10 zaidi ya kiwango cha Sh.35,299 milioni kinachotegemewo kukusanywa ifikapo Juni, 1993. Mikakati itakoyotumika ili kufikia lengo hilo ni pamoja na kuendelea kudhibiti uuzoji nje, no uingizaji bidhaa ili kuhakikisha kuwa wote wanohusika wanalipa kodi zinazostahili. Uundaji wo Idaro mpya yo Upelelezi unategemewo pamoja no majukumu mengine kusaidia kuzuia magendo no uhalifu kotiko ukusanyaji mapato. Hatua za kisheria no kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wale walipa kodi wanaokwepa wajibu woo pamoja no wotumishi wachache wasiokuwa waaminifu.

## Idara ya Kodi ya Mapato

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 Idara ya Kodi ya Mapato ilipangiwa kukusanya jumla ya Sh.44,735 milioni kutokana na Kodi ya Mapato, na Idara yenyewe ilijiwekea lengo la ndani la Shs.47,500 milioni. Takwimu za awali zinaonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 1993 makusanyo yalifikia Sh.47,396 milioni zikiwa ni Sh.2,661 milioni au asilimia 5.9 ya lengo lililowekwa, ingawa ni pungufu kidogo kulinganisha na malengo ya ndani ya Idara. Hivyo, pamoja na hali mbaya ya uchumi iliyosababishwa na upungufu wa umeme, idara hii ilijitahidi na kuweza kukusanya kiwango hicho. Mafanikio haya yamefikiwa kutokana na watumishi wa idara kufanya kazi kwa uadilifu na ufanisi kufuatia mikakati iliyowekwa na Idara ya kukusanya malimbikizo ya kodi za nyumba, kuhakikisha waajiri wanawasilisha Idarani makato ya 'PAYE. Payroll Levy' na 'Withholding tax' kwa wakati wake. Idara ya Kodi ya Mapato pia ilikusanya na kufanyia uchambuzi takwimu za walipa kodi katika sekta mbalimbali ili kuhakikisha wanalipa kodi kufuatana na sheria.

17. Katika mwaka wa fedha 1993/94, Idara imepangiwa kukusanya Sh.58,614 milioni ambayo ni Sh.11,218 milioni au asilimia 24 zaidi ya kiwango kinachotegemwa kukusanywa ifikapo Juni, 1993. Makadirio hayo yanahusisha yale ya Kodi ya Mapato Sh.52,026 milioni na "Specified Buildings Act" ya 1993 ya Sh.6,585 milioni inayotarajiwa kuanza rasmi hapo tarehe 1 Januari, 1994. Mikakati itakayotumika ili kufikia lengo hilo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa kumbukumbu za walipa kodi wote na kuhakikisha kuwa kila mmoja analipa kodi kwa mujibu wa sheria. Idara kwa kushirikiana na Idara mpya ya Upelelezi itachunguza kwa makini tabia ya ukwepaji kodi na kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu walipa kodi na watumishi wanaohusika pale wanapobainika.

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 Baraza la Rufaa za Kodi ya Mapato (National Tax Appeals Board) liliendelea kusikiliza malalamiko ya walipa kodi.

Takea Baraza lianzishwe mwaka 1982 limeandikisha jumla ya rufaa 647. Katika kipindi hicho rufaa 575 zimesikilizwa na kumalizika. Kati ya rufaa 72 zilizobaki, rufaa 10 zimesikilizwa na kumalizika katika mwaka wa 1992/93, rufaa nyingine 26 zinaendelea kushughulikiwa hivi sasa baada ya kukamilisha taarifa muhimu zinazohitajika. Maandalizi ya awali ya rufaa 36 zinazobakia yataanza pia 1993/94. Katika kipindi hiki Baraza limekuwa na Vikao Dar es Salaam, Kilimanjara, Arusha na Mara.

## Idara ya Kodi ya Mauzo na Kodi za Ndani.

19. Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza Idara hii imeundwa hivi karibuni kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Kodi zinazohusika ni zile zote zinazotozwa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na ada mbalimbali kama ada za leseni za biashara na ada za usafiri wa magari.

Majukumu ya Idara hii yatakuwa ni kukusanya Ushuru wa 'Excise Duty' kwa bidhaa za ndani, kukusanya kodi ya mauzo kwenye bidhaa zinazazalishwa humu nchini, kukusanya kodi nyinginezo ikijumuisha ushuru na ada pamoja na ukusanyaji wa mapato yasiya ya kodi (Non-Tax Revenue) ambayo hujumuisha ada na mapato yatokanayo na kunadi bidhaa zinazohadhiwa na Idara, mauzo ya mitambo, magari na vifaa chakavu vya Serikali.

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1993/94 Idara ya Kadi ya Mauza imepangiwa kukusanya Sh.56,100 milioni, kutakana na vianzio mbalimbali vya kodi inazokusanya. Ili kufikia lengo hila juhudi zitaelekezwa katika kudhibiti uzalishaji viwandani ili kuhakikisha kuwa wote wanaahusika wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria. Idara inategemea kuwa karibu na Idara mpya ya Upelelezi kwa nia ya kuwabana watumishi na walipa kodi wasia waominifu na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria pale inapobainika.

21. Mheshimiwa Spika, shughuli ya upelelezi katika idara za kodi imekuwa ikizorota mwaka hadi mwaka kwa sababu mbalimbali. Matokeo yake ni udanganyifu na ukwepaji mkubwa wa kodi mbalimbali ambao umeathiri bajeti ya Serikali kwa kiwanga kikubwa. Ili kurejesha shughuli hii kwenye kiwango kinachotakiwa Serikali imeamua kuunda idara kamili ya upelelezi inayaongozwa na Kamishna kwenye Makao Makuu ya Wizara. Kazi kubwa ya idara hii itakuwa kufuatilia kwa kina nyenda za walipa kodi mbalimbali kwa kushirikiana na vyombo vya dola, kuchambua maelekeo katika vianzio muhimu vya kodi, kutoa msaada wa kiupelelezi kwa idara zote za kodi na kushauri Wizara ipasavyo. Idara hii pia itakuwa silaha muhimu dhidi ya tishio linalozidi kuonekana la Nchi yetu kutumiwa kama kituo cha kupitishia madawa ya kulevya. Mheshimiwa Spika, shughuli za kufuatilia na kusaka wakwepa kodi na wanaojihusisha na madawa ya kulevya inahitaji watu wenye ujuzi na nyenzo za

kufanyia kazi hizo, hivyo, Idara itawajibika kufunza wafanyakazi na pia ipatiwe nyenzo zinazatakiwa kufanya shughuli hizo.

**Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Serikali**

22. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kuwa udhibiti wa matumizi ya Serikali katika Wizara na Mikoa umelegalega kwa kiasi kikubwa. Wizi wa fedha na ubadhirifu kwa kutumia mbinu mbalimbali pamoja na ukiukaji wa viwango vya bajeti ni baadhi ya ishara zake. Ili kuimarisha udhibiti, Hazina imetoa tena Waraka mwingine kwa Maafisa Wahasibu kuelekeza umuhimu wa udhibiti na athari za kiuchumi zinazotokana na uvukaji holela wa viwango vya bajeti. Kadhalika Waraka huo umefafanua hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wale watakaohusika na uvukaji wa viwanga kwa mwaka 1993/94.

23. Mheshimiwa Spika, harakati za kubaresha uwekaji wa hesabu za Serikali na udhibiti wa makusanya ya Mapato na Matumizi ya Serikali, zilianza miaka kadhaa iliyapita. Mwaka 1988/89 Hazina ilinunua na kusambaza kwa kila Afisa Mhasibu Kampyuta (Personal Computers.) Hadi sasa, Kampyuta hiza zilikuwa zinatumika kwa kiasi kidaga sana ukilinganisha na uweza wake. Kuanzia mwaka 1993/94 zinaandaliwa Programu za kupanua matumizi ya Kampyuta hizi ili kutimiza azma ya kubaresha udhibiti na hali ya mahesabu ya Serikali. Ni mategemea yangu kwamba azma hiya itatimizwa katika muda mfupi ujaa.

24. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine inayakusudiwa kuchukuliwa ili kuangeza udhibiti wa matumizi, ni ile ya kuanzisha utaratibu wa "Sub-treasuries". Utaratibu hua unafanana sana na ule uliakuwepa miaka ya nyuma wa "Internal Revenue Offices".

Kwa hiyo katika mwaka wa fedha 1993/94 utekelezaji wa mradi wa "Sub-treasuries" utaanza kwa majaribio kwenye vituo vinne vilivyoteuliwa. Faida za kuwa na Sub-treasuries zinatazamiwa kuwa kama ifuatavyo;-

(i) Kuimarisha udhibiti kwa kupunguza vituo vya malipo na mapokezi ya maduhuli.

(ii) Kudhibiti matumizi kwa kuwa hapatakuwa na malipo yasiyo na fedha yatakayopitishwa, hivyo kupunguza matumizi makubwa ya ziada bila idhini ya Bunge.

(iii) Kurahisisha utekelezaji wa hatua inayofuata ya "full computerization".

Matokeo ya majaribio kwenye vituo vilivyoteuliwa yatasaidia kuweka vigezo vya uamuzi wa Serikali kuhusu kuendeleza mfumo huo ili utumike katika Mikoa yote mwaka 1994/95.

Utaratibu huu utahusisha pia Wizara zote. Hatimaye malipo yote na makusanya ya Wakurugenzi wa Mikoa, Wizara na Idara zingine katika Mikoa yatakuwa yakifanyika na "Sub-treasuries" zitakazoundwa.

## Halmashauri Kuu ya Tenda

25. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1993/94 Halmashauri Kuu ya Tenda iliendelea vizuri na shughuli yake ya kusimamia tenda za serikali na kutoa ushauri juu ya manunuzi. Jumla ya tenda 58 ziliitishwa na kuamuliwa katika vikao 19 vya Halmashauri. Tenda hizo zilijumuisha zile za kimataifa na zile za humu nchini. Matatizo yaliyokabili shughuli za Halmashauri Kuu ya Tenda ni pamoja na yale yatokanayo na Wizara na Mikoa kuchelewa kutuma mahitaji yao, Maafisa Wahasibu kutojihusisha vya kutosha kwenye tenda zinazowahusu, na kutozingatiwa vya kutosha vipengele vya mikataba ya tenda.

26. Mheshimiwa Spika, ili kuweka msukumo maalum katika kazi ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini, Serikali, kwa kushauriana na Benki ya Dunia, iliunda Kamati ya Tenda ya Taifa kwa ajili ya kazi hiyo. Mnamo mwaka 1992/93 kamati hiyo ilipokea tenda 31. Kati ya hizo tenda 21 ziliamuliwa na zilizosalia 10 zilirejeshwa mikoani zilikoanzia ili ziweze kufanyiwa tathmini upya kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo.

27. Mheshimiwa Spika, jukumu jingine la wizara yangu ni kuhakikimali kama ilivyo katika 'Exchequer and Audit Ordinance' ya mwaka 1961. Katika mwaka 1992/93 Wizara ilitarajia kufanya uhakikimali katika Ofisi 180 za Wizara, Idara na Mikoa. Hadi kufikia mwisho wa 1992/93 Wizara imepokea jumla ya taarifa 230 na hivyo kuvuka lenga lililowekwa. Wizara imekuwa ikitoa semina na mafunzo kuhusu uimarishaji wa uhakikimali Serikalini.

Vilevile kanuni za fedha zinazohusu ununuzi wa vifaa ziliendelea kufanyiwa marekebisho ili zilingane na wakati. Wizara pia ilisimamia zoezi la uuzaji wa mali na vifaa chakavu vya Serikali. Katika mwaka 1993/94 Wizara inatarajia kuhakiki Ofisi 225 katika Wizara, Idara na Mikoa. Wizara inatarajia kutoa mafunzo na semina katika nyanja ya ugavi na fani nyinginezo ili kudhibiti utunzaji wa mali na vifaa vya Serikalini.

**Huduma za Kompyuta.**

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 huduma ya Komputa imeeendelea vizuri. Kazi hizo ni pamoja na kutayarisha mishahara ya kila mwezi ya watumishi wote wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kutayarisha malipo ya kila mwezi ya pensheni za Serikali, kuweka mahesabu ya michango ya wanachama wa "Government Employees Provident Fund" (GEPF) na kuweka mahesabu ya mikopo ya Serikali kwa Mashirika yote.

## Huduma za Malipo ya Uzeeni.

29. Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara ya Fedha ni kutoa huduma za malipo ya uzeeni kwa watumishi wa Serikali, Walimu, Wanajeshi, Viongozi wa Ngazi za Juu wa Serikali na Viongozi wa Siasa. Katika mwaka 1992/93 wastaafu 5445 wakiwemo waalimu 810, wanajeshi 1,065 na watumishi wengine 3,570 walishughulikiwa na kupewa malipo yao ya Uzeeni. Shughuli hizi zimeongezeka kutokana na uamuzi wa Serikali wa kupunguza watumishi wake. Katika kipindi cha 1992/93 wastaafu 8,902 walihusika katika zoezi la Serikali la kupunguza watumishi wake. Hawa ni tofauti na wale wastaafu wa kawaida.

30. Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inaangalia mwelekeo mpya wa Pensheni na kuona ni jinsi gani mstaafu anaweza kuhudumiwa haraka bila ya kuchelewesha malipo yake.

Wizara itafanya mawasiliano ya karibu na Idara Kuu ya Utumishi na Wizara nyingine ili kuwaandaa wanaokaribia kustaafu na kuwashughulika mapema wakati wakiwa bado kazini. Serikali pia imeamua kuongeza kiwango cha kulipa pensheni kwa mkupuo kutoka kiwango cha sasa cha Sh.1,500/= mpaka kufikia Sh.3,000/=. Hivyo, wastaafu wapato 3,900 watanufaika na zoezi hili. Nia ya Serikali ya kulipa pensheni kwa mkupuo mmoja haina maana ya kukwepa jukumu lake la kuwahudumia wastaafu bali ni kutaka kuwapunguzia kero ya kufuata malipo madogo madogo kila mwezi kwa gharama kubwa. Mheshimiwa Spika, tangu zoezi hili la kulipa pensheni kwa mkupuo mmoja lianze wastaafu wapatao 9,672 wameshalipwa haki zao.

**Sekta ya Mashirika ya Umma.**

31. Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekuwa likielezwa matatizo kadhaa ambayo yamekuwa yakiathiri ufanisi katika Mashirika ya Umma.

Baadhi ya matatizo haya yalitokana na upungufu wa mitaji, ukwasi duni, mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya fedha yetu, ambako kumezidisha ukubwa wa madeni ya Mashirika na hasa madeni yaliyo katika fedha za kigeni. Uchambuzi uliofanywa ulionyesha kuwa Serikali haina uwezo wa kuyakabili matatizo yote haya kifedha. Kutokana na hali hiyo Serikali imeamua kupunguza mzigo wa gharama za kuyaendesha Mashirika haya kwa kurekebisha mfumo wake wa sasa. Baadhi ya Mashirika yataingizwa kwenye ubia na sekta binafsi, mengine yatauzwa na yale yenye matatizo sugu na hali mbaya mno yatafilisiwa. Kama inavyofahamika, vyombo viwili viliundwa kusimamia utekelezaji wa shughuli hii. Vyombo hivyo ni Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Mashirika ya Umma kwa upande mmoja na Mdhamini wa Madeni (LART) kwa upande mwingine. Vyombo vyote vimeshaanza kazi zake rasmi.

32. Tume, kwa upande wake, imekwishachambua na kuweka kumbukumbu muhimu za Mashirika mengi zinazoonyesha

ukwasi wa Mashirika hayo, thamani ya mali zake na idadi ya wafanyakazi wao. Kumbukumbu hizi, zitasaidia Tume katika kupima uwezo wa Mashirika hayo kuendesha shughuli zake kwa ufanisi na faida. Vile vile, katika mpango wake wa awali Tume inajiwekea lengo kwamba hadi ifikapo mwezi Desemba, 1994 Mashirika 105 yatakuwa yamekwisha shughulikiwa kwa namna moja au nyingine. Ni nia ya Serikali kurekebisha mfumo wa idadi kubwa ya Mashirika ya Kibiashara katika kipindi cha miaka mitano. Kwa miaka miwili ya kwanza, Tume imeyapa kipaumbele Mashirika ambayo:-

(i) Yanaweza kurekebishwa kwa urahisi na yakaweza kujiendesha kibiashara na kwa ufanisi zaidi;

(ii) Yanapata hasara kiasi cha kuifanya Serikali itumie gharama kubwa kwa kuyahudumia, hivyo kuleta uwiano mbaya kati ya mapato na matumizi ya Serikali kwa jumla;

(iii) Ni madogo na ambayo uuzaji wake unaweza kufanywa kwa urahisi na hivyo kuharakisha utekelezaji wa zoezi hili.

(iv) Yalikuwa yamekwishafanyiwa uchambuzi wa awali kisekta na Kamati ndogo za Wizara. Sekta hizo zinajumuisha Sekta ya Ngozi, Nguo, Mafuta ya kupikia, Vifaa vya Ujenzi, na Viwanda vya Chuma na Uhandisi. Aidha, Tume imekwishafanya tathmini ya awali ya Mashirika ambayo yatategemewa kuendeshwa kwa mikataba maalum (performance contracts) na Serikali. Mashirika machache yaliyochaguliwa kuanza ni Shirika la Posto na Simu, Shirika la Umeme, Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Kiwanda cha Nguo cha Mwanza (MWATEX) na Kiwanda cha Nguo cha Musoma (MUTEX).

Kwa Jumla Tume bado inaendelea na zoezi hili la kurekebisha mfumo wa Mashirika ya Umma na mapendekezo yatakuwa yakitolewa hatua kwa hatua.

33. Mheshimiwa Spika, eneo lingine kubwa lenye matatizo kwa Mashirika yetu ya Umma ni suala la madeni. Baadhi ya Mashirika yameelemewa na madeni mengi sugu yasiyolipika. Baadhi ya madeni haya yamekopwa kutoka katika Mabenki yetu ambaya kwa sasa yamekwishaingia katika ushindani wa kibiashara. Ni jukumu la Serikali kuyaimarisha mabenki haya ili yaweze kuhimili ushindani huo. Mdhamini wa Madeni (LART) kwa upande wake anatakiwa arithi madeni haya kwa niaba ya Serikali ili kuyaondolea mzigo huo mabenki. Hadi sasa, Mdhamini wa Madeni alikuwa amekwishachambua madeni ya baadhi ya mashirika na kurithi madeni yenye thamani ya Sh.435.6 milioni kutoka Mashirika matano yaliyokopeshwa na CRDB na kiasi cha Sh.13,121.5 milioni kutoka kwa Mashirika 22 yaliyokopeshwa na NBC.

Serikali kwa kupitia Benki Kuu imekwishachapisha dhamana (Bonds) ambazo zitatumika katika kulipia madeni hayo. Kadhalika, LART katika kushughulikia namna ya kupata marejesho ya fedha hizi, imeandaa taratibu (LART Seisure and Disposal Rules 1993) pamoja na miongozo (LART Operating Procedures and Guidelines for Recovery of the Non-performing Assets) itakayotumika katika kudai au kufilisi Mashirika yanayohusika. Taratibu hizo zitatangazwa katika Gazeti la Serikali hivi karibuni.

34. Ingawa jitihada zinafanyika katika kulikabili tatizo la madeni sugu ya Mashirika yaliyokopeshwa na mabenki yetu, juhudi kubwa zaidi bado zinahitajika katika kuyakabili madeni mengine ya Mashirika waliyoyakopa katika fedha za kigeni na kudhaminiwa na Serikali. Hivyo, Serikali kama mdhamini, inakabiliwa na mzigo mkubwa wa kuheshimu dhamana hizo ambazo ilipofikia Juni 30, 1992, zilikuwa Shilingi bilioni 238.7.

Vile vile, Mashirika yenyewe yamekuwa hayana utamaduni wa kulipana madeni yao. Hali hii imesababisha mashirika mengi kuwa na madeni makubwa, wakati hua hua mashirika haya naya yanadai Mashirika mengine. Tatizo hili la madeni ya Mashirika linaweza kutanzuliwa kwa kubadilisha mikopa na kuwa mtaji, kuahirisha malipa au Serikali kuchukua madeni haya pale itakapoana itawezesha au kurahisisha majadiliano ya uuzaji wa Shirika linalohusika. Tume inaendelea kuyashughulikia madeni ya kila Shirika kufuatana na hali ya Shirika lenyewe wakati ikirekebisha mifumo ya mitaji ya Mashirika haya.

**Utawala na Utumishi.**

35. Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kuendeleza na kuimarisha shughuli za Utawala na Utumishi, Wizara yangu imerekebisha miundo yote 21 ya Utumishi ya kada tunazosimamia na imeanzisha miundo miwili

mipya kwa ajili ya kada ya Wakaguzi wa hesabu wa Ndani na Wachunguzi wa Hesabu wa Ndani (Internal Examiners of Accounts). Marekebisho hayo pia yanakusudia kuweka mazingira yenye kuvutia watumishi waliopo na kutoa nafasi kwa wataalam wapya kujiunga na Wizara pindi ikibidi. Hivyo, katika mwaka 1993/94 Wizara yangu itaendelea kusisitiza juu ya upatikanaji wa taarifa za siri za utendaji kazi kwa watumishi wote ili hatua za kuwapandisha vyeo watumishi wenye stahili kwa mujibu wa miundo hii mipya zichukuliwe kwa wakati unaotakiwa.

36. Mheshimiwa Spika, ili kujenga imani ya watumishi katika kazi zao, kukuza na kuimarisha vipaji pamoja na ubingwa wao, mafunzo yatatiliwa mkazo mkubwa. Kwa kutambua umuhimu huu, Wizara yangu inaendelea kutoa nafasi kwa watumishi wake kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu humu nchini na nje.

Katika mwaka wa fedha 1993/94 Wizara yangu inakusudia kuwapa mafunzo watumishi wengi zaidi kulingana na uwezo wetu kwa mujibu wa fedha zilizokasimiwa na misaada itakayotolewa na wahisani mbali mbali. Pamoja na juhudi hizi za mafunzo Wizara yangu inasimamia pia shughuli za Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IMF), Chuo cha Kodi (ITA), na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

**Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA)**

37. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam, pamoja na Matawi yake matatu yaliyoko Mbeya, Singida na Mtwara, kitaendelea na jitihada zake za kutumia mbinu na mikakati mbalimbali ili kupunguza tatizo la uhaba mkubwa wa wataalam katika fani za uhasibu na utunzaji vifaa (Ubaharia) nchini.
Uwezo wa Chuo ni kuchukua wanafunzi 910 kwa mwaka katika kozi mbalimbali za Uhasibu na Ubaharia.

Mnamo mwaka 1992/93, Chuo kilichukua jumla ya wanafunzi 825 katika kozi mbalimbali za Uhasibu no Uboharia katika ngazi za cheti cha Stashahada. Chuo katika jitihada zake za kuongeza wataalam katika fani hizo katika mwaka huo huo 1992/93 kiliendesha kozi mbalimbali za Uhasibu na Uboharia za masomo ya jioni kwa wanafunzi 628. Kwa mwoka 1993/94 lengo la Chuo ni kuchukua wanafunzi 900 katika kozi mbalimbali za Uhasibu na Uboharia. Hali kadhalika, katika mwaka huu Chuo kinategemea kuendesha kozi za masomo ya jioni kwa wanafunzi 650 katika fani hizo.

Chuo Cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

38. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kina jukumu la kuendeleza foni za Benki, Bima, Usimamizi wa Fedha, Uhasibu, hifadhi ya jamii, usimamizi wa kodi no foni nyingine zinazohusiana na taaluma ya usimamizi wa fedha.

Katika mwaka 1992/93 Chuo kilipanga kuongeza idadi na ubora wa wahadhiri kitaaluma ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza lengo hilo, Chuo kimefanikiwa kuajiri Wahadhiri wapya 14 badala ya 10 kama ilivyotarajiwa na kupeleka Wahadhiri 9 masomoni kwa shahada ya pill (Masters). Lengo lingine lilikuwa kuimarisha kazi ndefu na fupi kwa kuongeza idadi ya washiriki katika kazi hizo, pamoja na kubaresha mapata na mitaala ya kazi zake ili ziende na wakati. Katika mwaka 1992/93 Chuo kimefanikiwa kusajili wanafunzi 918, ambalo ni ongezeko la wanafunzi 18 au asilimia 2 ya lengo. Hadi kufikia Machi, 1993 kazi fupi zilikiingizia Chuo mapato ya Shilingi 132 milioni na matarajio yalikuwa ni kupata Shilingi 160 milioni ifikapo Juni, 1993. Hili ni ongezeko la asilimia 70 ya lengo.

39. Katika mwaka 1993/94 Chuo kitaendeleza jitihada zake za kubaresha mitaala.

Kuna mipango pia ya kuimarisha Utafiti na Uchapishaji, kuanzisha kozi za Kompyuta, kuanzisha kozi ya shahada ya Juu katika Usimamizi wa Fedha (M.Sc. in Finance), ukamilishaji wa ukarabati wa majengo ya Chuo, kutoa ushauri (Consultancy) na kuweka vitega uchumi kwa njia ya Ubia. Kwa Jumla Chuo kinatarajia kusajili wanafunzi 1019 mwaka huu wa fedha.

## Chuo cha Kodi (ITA)

40. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya utendaji kazi kwa watumishi wa Idara za Kodi, Chuo cha Kodi kimechangia kwa kiasi kikubwa katika kufonikisha malengo ya Idara zinazokusanya kodi. Katika kufanikisha malengo ya Idara hizo, Chuo kilipanga kuendesha kozi ndefu na fupi nne za mafunzo ya awali (Basic Courses) na kozi fupi maalum (Specialized) sita za wiki mbili hadi sita. Watumishi 200 walishiriki katika kozi hizo.

Hata hivyo idadi hii bado ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji. Matatizo yaliyoathiri shughuli za Chuo hiki ni pamoja na uhaba wa vitendea kazi, upungufu wa madarasa na ukosefu wa jengo la Maktaba. Ili kukabili matatizo haya Chuo kinatarajia kufanya upanuzi wa majengo kulingana na uwezo wa kifedha, ili kiwe na Maktaba, madarasa zaidi, afisi kwa walimu na zahanati. Chuo kinatarajia kuendesha kazi na warsha zaidi ili kukidhi mahitaji ya Idara za kadi.

**Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)**

41. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uhasibu Arusha kina jukumu la kuongeza idadi ya wataalam wa uhasibu katika ngazi zote na hasa ngazi mbili za juu kabisa yaani "Professional Levels III na IV". Kufuatana na utafiti uliofanywa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), bado kuna pengo la zaidi ya asilimia 60 katika mahitaji ya wahasibu wa ngazi zote tatu, yaani, "Technician Level",

"Semi-Professional Level" na "Professional Level". Katika mwaka 1992/93 Chuo kiliingiza wanafunzi 72. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na uwezo wa Chuo wa kupokea wanafunzi zaidi ya 150. Katika mwaka 1993/94 Chuo kinategemea kuongeza idadi ya wanafunzi hadi kufikia zaidi ya 150. Aidha, ili kujiongezea mapato Chuo kinategemea kujishughulisha na ushauri "Consultancy", uendeshaji wa kozi fupi kwa "Practising Accountants", na ukodishaji wa mabweni na madarasa kwa watakaohitaji hasa wakati wa likizo.

## Mashirika ya Fedha

42. Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha ina umuhimu wa pekee kwa wakati huu ambapo juhudi za kurekebisha sekta ya umma na uchumi wetu kwa jumla zinaendelea. Katika mwaka 1992/93 hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kurekebisha sekta ya fedha (Financial Sector Restructuring).

Maenea hayo ni pamaja na kubadilisha mifumo ya Benki zetu ili kujizatiti kwa ushindani katika eneo hili, kusafisha mizania za Benki hizi hasa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB), ili kuziwezesha kufanya shughuli zao kibiashara. Katika mwaka 1993/94 Serikali inakusudia kuhusisha kwenye marekebisha hayo Benki ya Nyumba (THB), Benki ya Rasilimali (TIB), na Shirika la Bima (NIC) kwa nia ya kuviwezesha vyombo hivi navyo kukabiliana na ushindani wa kibiashara katika nyanja zao.

43. Kutokana na kupitishwa kwa Sheria ya Mabenki ya mwaka 1991, Wizara ya Fedha itaendelea na jukumu lake la kusimamia vyambo hivyo vya fedha, ili kuhakikisha kuwa shughuli zao zinalingana na matarajio ya Serikali na Taifa kwa jumla, katika kuruhusu uanzishaji wake. Hivyo lengo kuu litaendelea kuwa ni kuwezesha utaoji wa huduma bora kwa wananchi katika hali ya ushindani wa vyombo vya fedha.

## Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

44. Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutoa huduma za ushauri na kutoa mchango katika usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa kurekebisha uchumi ulioanza mwaka 1986, hususan katika fani ya kurekebisha mfumo wa sekta ya fedha. Urekebishaji wa sekta hiyo katika nyanja za mifumo ya sheria na sera, mabadiliko katika mfumo wa mabenki na vyombo vya fedha, ukuzaji wa uwezo wa utendaji kazi, na sera za kifedha kwa jumla ni kati ya mambo yaliyoendelea kutekelezwa. Katika kutekeleza sera ya kifedha, Benki Kuu, iliendelea kubuni taratibu za kisasa za kuboresha huduma za kibenki ili kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya uchumi na ya umma kwa ujumla.

45. Mheshimiwa Spika, kwa nia ya kutekeleza kwa ufanisi zaidi sera huria ya kifedha na pia kupunguza mikopo ya Serikali kutoka kwenye mabenki ambayo

ina athari kubwa kwa uchumi, Benki kuu imekwishafanya matayarisha ya kutasha na imekwishaanza kutekeleza mpanga ya uuzaji wa dhamana za muda mfupi (Treasury Bills) kwa njia ya minada (auctions) katika mwaka wa fedha wa 1993/94. Minada hiyo itahusisha mabenki, vyamba vingine vya fedha, mashirika ya umma na watu binafsi. Mpanga wa kuwa na wakala hasa mabenki na vyamba vingine vya kifedha katika minada hii utaanzishwa baadaye ili kuwafikia wanunuzi wadaga wadaga kwenye maenea mbali mbali nchini.

46. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuweka misingi imara ya utaaji leseni kwa mabenki mapya pamaja na mipanga ya usimamizi unaatakiwa, yalikamilika katika kipindi cha mwaka 1992. Kutakana na maendelea haya, Benki Kuu iliweza kutaa leseni za kuanzisha huduma za benki kwa Standard Chartered Bank Tanzania Ltd. na Meridien Biaa Bank (T) Ltd. ambaza zilitegemewa kuanza kazi katika raba ya kwanza ya mwaka huu wa fedha wa 1993/94.

Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Meridien Biao Bank tayari imekwishaanza kufanya kazi tangu tarehe 9/8/93. Pia benki mbili za nje, yaani Benki ya Biashara ya Kenya na Belgolaise Bank zilifungua afisi zao za uwakilishi nchini. Benki Kuu pia inaendelea kupokea maombi ya vyombo vinavyotaka kuanzisha huduma za fedha hapa nchini.

47. Mheshimiwa Spika, umuhimu wa mabenki kuwa na mitaji inayotosheleza kulingana na sheria ya Mabenki na vyombo vya kifedha ya mwaka 1991 umetiliwa mkazo. Hivyo, Benki Kuu ilisimamia utekelezaji wa uamuzi wa Serikali wa kuzipa tena mitaji (Recapitalize) benki zetu na kusafisha mizania yao kupitia (LART). Awamu ya kwanza ya kuimarisha mitaji hiyo ilikuwa kwa njia ya dhamana za Serikali za muda mrefu zenye thamani ya Shilingi 72,494,184,000 kwa NBC na Shilingi 16,995,094,000 kwa CRDB mwezi Juni, 1992.

Awamu ya pili inategemewa kutekelezwa kabla ya mwezi Oktaba, 1993 ili kutimiza mahitaji ya sheria ya mabenki ya 1991. Aidha, hatua za kurekebisha TIB, THB na PBZ zimeanza kutekelezwa.

48. Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imeendelea kubuni na kushauri Serikali kuhusu sera madhubuti katika usimamizi na utekelezaji wa taratibu huria za fedha za kigeni. Katika kipindi cha mwaka 1992/93, Benki Kuu ilitoa leseni za kuendesha maduka ya kubadilisha fedha za kigeni (Bureau de Change). Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 1993, maduka 70 ya fedha za kigeni yalikuwa yanafanya kazi kote nchini kati ya zaidi kidogo ya 100 yaliyopewa leseni. Tangu maduka haya yalipoanza mwezi Aprili 21, 1992 hadi mwisho wa Juni 1993, jumla ya fedha za kigeni zilizonunuliwa na maduka haya ilifikia kiasi cha dola za Kimarekani 222 milioni wakati fedha za kigeni zilizouzwa na maduka haya zilifikia dola 200 milioni, na kuleta ziada (net inflow) ya dola 22 milioni katika kipindi hicho.

Kwa maana hiyo maduka haya yanatuletea fedha za kigeni.

49. Kwa kutekeleza sera ya Serikali ya kulegeza zaidi masharti ya uagizaji bidhaa nchi za nje, idadi na aina ya bidhaa zinazohitaji vibali maalum (negative list) kwenye mpango wa OGL ilipunguzwa, na kubakiza bidhaa zile tu zinazodhibitiwa kwa sababu za kiafya, usalama, na kulinda maliasili, pamoja na bidhaa za anasa (luxury goods).

50. Mshehimiwa Spika, kwa kushirikiana na matawi ya Benki ya Taifa ya Biashara pamoja na Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini, Benki Kuu pia iliendelea kununua dhahabu. Katika kipindi cha mwaka 1992/93 kiasi cha tani 4.5 za dhahabu ghafi kilinunuliwa na kufikisha jumla ya dhahabu iliyonunuliwa tangu mpango huu uanze (Aprili 1990) kukaribia tani 12. Ni dhahiri, zoezi hili la ununuzi wa dhahabu limesaidia kuongeza akiba ya fedha za kigeni (foreign reserves) ya nchi.

51. Mheshimiwa Spika, mpango wa kubadilisha madeni "Debt Conversion Programme" ulioanzishwa Desemba 1990 uliendelea mpaka mwisho wa Juni, 1993. Lengo la mpango huu lilikuwa kupunguza mzigo wa kulipa madeni yetu ya nje kwa kuyabadilisha kwa njia ya kuweka vitega uchumi kwenye sekta muhimu za uchumi hapa nchini. Katika kipindi cha Januari, 1991 hadi Juni, 1993, madeni yenye thamani ya dola za Kimarekani 88 milioni yalibadilishwa kwa kutoa fedha ya Tanzania yenye thamani ya Sh.20,991.75 milioni ili kugharamia miradi iliyokubaliwa chini ya mpango huo. Katika mpango huu, sekta zilizofaidika mpaka sasa ni kilimo, utalii, viwanda, madini, biashara na ustawi wa jamii.

52. Mheshimiwa Spika, ningependa hapa kutamka kuwa mafanikio haya yote katika shughuli za Benki Kuu yalipatikana chini ya uongozi shupavu wa Marehemu Gilman Rutihinda aliyekuwa Gavana wa Benki hiyo katika kipindi cha miaka 4, hadi alipofariki tarehe 20/6/93.

Nina hakika sote tunaungana kumwomba Mwenyezi Mungu teno aiweke roho yake mahali pema peponi. Wakati huo huo Serikali ina mategemeo makubwa kuwa Benki Kuu itazidi kuimarika chini ya uongozi wa Dakta Idris Rashid ambaye ameteuliwa mwezi uliopita kuwa Gavana mpya. Benki imeendelea kusimamia na kufuatilia shughuli za utoaji na ulipoji mikopo ili kuhakikisha kwamba mikopa hiyo inatolewa kwa watu, Makampuni na vyombo vyenye uwezo wa kuitumia na kuiwezesha Benki kuwo na uhakika kuwa mikopa inayatolewa inarudishwa. Kutokana na mikakati hiyo wateja wameanza kurudisha mikopo iliyokwama hasa baada ya Benki kuanzisha zoezi la kuuza dhamana za wateja.

**Benki ya Taifa ya Biashara (NBC):**

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 Benki ya Taifa ya Biashara ilijiwekea lengo la kuongeza amana kwa asilimia 40, ikilinganishwa na mwaka 1991/92.

Hadi kufikia mwezi Machi 1993, kiasi cha Sh.215,456 milioni zilikuwa zimekusanywa kama amana ikiwa ni angezeka la asilimia 70 kwa miezi tisa ya kwanza ya 1992/93. Tegemeo la mwaka mzima ni angezeka la asilimia 45 ukilinganisha na lenga la asilimia 40. Mikapa ya muda mrefu na muda mfupi iliyakuwo imetalewa katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ilikuwa Sh.146,163 milioni na kuufanya uwiana wa mikopa na amana kufikia asilimia 68. Aidha, katika kipindi hicha mapata yalikuwa yamefikia Sh.27,925 milliani ambapo matumizi yalikuwa yamefikia Sh.26,569milliani. Mikapo isiyolipika iliyotolewa kwenye faida, ilifikia kiasi cha Sh.11,420 milioni na kufanya Benki ipate hasara ya Sh.10,064 milioni kwa miezi tisa ya kwanza.

54. Mheshimiwa Spika, kufuatia Muswada wa Sheria wa mwaka 1991 unaahusu mabenki na vyambo vingine vya fedha, Benki tokea tarehe 1 Julai, 1992 imeanza kutekeleza miangazo ihusuyo muunda wa kifedha

"Prudential Guidelines on Management of Risk Assets, Classification of loans and other Risk, Provisioning for losses and Accrual of Interests". Mikopo iliyokuwa imekwama ilihamishiwa LART wakati ambapo Serikali litaa dhamana kwa Benki kutakana na mikopo hiyo.

55. katika kipindi cha mwaka 1993/94 , Benki ya Taifa ya Biashara imepanga kuendeleza na kubaresha huduma zake ili Benki hiyo iweze kubakiza asilimia 75 ya soko katika kipindi cha ushindani. Harakati hiza ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake pamoja na uimarishaji na uanzishaji wa matumizi ya Kompyuta ili kujizatiti kwa ushindani na Benki nyingine zinazaanzishwa. Pia mkaza utawekwa katika shughuli za usambazaji wa huduma za kibenki ili kuangeza amana (deposits) kwa asilimia 50. Benki itaweka uwiano wa ukwasi kuwa asilimia 20 ya jumla ya amana na kwamba uwiano kati ya matumizi na mapato hauzidi asilimia 60.

Benki inatazamia kuanza na kutumia Kampyuta katika Matawi 13 katika mwaka 1993/94. Aidha, uandaaji na hatua za utayarishaji wa hati mbali mbali utarahisishwa ili kuongeza ufanisi.

**Benki ya Rasilimali (TIB)**

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 Benki ya Rasilimali (TIB) ilikopesha jumla ya Shilingi 79.7 milioni kinyume na lengo lake la kukopesha kiasi cha shilingi 1,000 milioni. Kiwango hiki kidogo cha ukopeshaji kimetokana na Benki kutopata fedha kutoka Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa pamoja na malimbikizo ya madeni kutoka kwa wateja wake, ambayo yalifikia Shilingi 10,200 milioni mwishoni mwa mwaka 1991/92. Hadi kufikia Desemba 31, 1992 Benki ilifanikiwa kukusanya Shilingi 1,051 milioni ikiwa ni asilimia 139 ya lengo lake la kukusanya Shilingi 756 milioni kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 1992.